JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAFUNZO YA VIONGOZI KATIKA NGAZI YA KIJIJI, MTAA NA KITONGOJI

HIFADHI ENDELEVU YA MAZINGIRA

7

DODOMA
APRILI, 2001

YALIYOMO

Uk.

Yaliyomo ii

HIFADHI ENDELEVU YA MAZINGIRA

1. Utangulizi.....1

2. Umuhimu wa Hifadhi ya Mazingira katika shughuli za Maendeleo..... 2

3. Vyanzo vya Uharibifu wa Mazingira..... 6

4. Athari Kutokana na Uharibifu wa Mazingira..... 8

5. Mbinu Endelevu za Kuhifadhi Mazingira Vijiji/Mijini..... 9

6. Wajibu wa Kiongozi wa Kijiji, Kitongoji na Mtaa katika Kuhifadhi Mazingira..... 11

7. Hitimisho..... 13

HIFADHI ENDELEVU YA MAZINGIRA

1. UTANGULIZI

Lengo la Serikali ni kumwezesha Kiongozi wa Serikali wa kuchaguliwa katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa kusimamia kikamilifu shughuli za hifadhi ya mazingira katika maeneo yao.

Mada hii inafafanua dhana ya hifadhi ya mazingira, sababu za uharibifu wake, namna ya kuyahifadhi na wajibu wa Kiongozi wa Serikali katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa katika kuhifadhi mazingira.

Maana ya Mazingira

Neno Mazingira lina maana pana sana. Mazingira yanahusu ardhi yetu, misitu yetu, maji tunayotumia na hewa tunayopumua, ambavyo vyote ni msingi wa maisha ya binadamu na viumbe wengine. Hivyo, hifadhi ya mazingira ni dhana pevu, ambayo hupelekea kwenye uwanja mpana unaounganisha hali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, na hata mila na desturi.

Maana ya hifadhi Endelevu ya Mazingira

Ili kuwepo na hifadhi endelevu wananchi wana wajibu wa kutunza mazingira yao na dhamana ya kuyahifadhi ipasavyo kwa ajili ya matumizi yao na vizazi vijavyo. Mafanikio ya hifadhi ya mazingira katika nyanja mbalimbali hutegemea sana elimu ya mazingira.

Kwa maana hii hifadhi endelevu ya mazingira lazima iambatane na hatua za makusudi za utoaji wa elimu ya mazingira kwa wananchi itakayowawezesha kuandaa na

kutekeleza mipango na miradi inayolenga katika kuhifadhi mazingira.

2. UMUHIMU WA HIFADHI YA MAZINGIRA KATIKA SHUGHULI ZA MAENDELEO

Pana uhusiano tegemezi kati ya uharibifu wa mazingira na umaskini. Uharibifu wa mazingira husababisha kuenea kwa umaskini; na umaskini mara nyingi husababisha uharibifu wa mazingira, kwani huwaondolea watu uwezo wa kusimamia rasilimali zao ipasavyo.

Mazingira na maendeleo ni vitu ambavyo haviwezi kutenganishwa. Pana mifano mingi na ya wazi kudhihirisha ambavyo shughuli nyingi za maendeleo ya kiuchumi na kijamii au matumizi ya maliasili kwa namna isiyozingatia athari zake, huweza kusababisha uharibifu wa mazingira.

Taratibu mbaya za kilimo, kama vile kufyeka ama kuchoma misitu, ukataji wa miti katika vyanzo vya maji huweza kuathiri ardhi kwa kuondoa rutuba ya udongo na kukausha maji.

Shughuli za uzalishaji mali katika viwanda mara nyingi huchangia kwa kiasi kikubwa katika uchafuzi wa mazingira ya ardhi, maji na anga, pale ambapo tahadhari haikuchukuliwa. Sehemu kubwa ya taka na maji machafu, rangi, plastiki na moshi hutokana na shughuli za viwanda. Viwanda huingiza uchafu mwingi katika mifumo ya maji machafu, ikiwa ni pamoja na kemikali zenye sumu. Vivyo hivyo kwenye sekta ya madini, mifugo na maeneo ya makazi.

Sekta zifuatazo zina uhusiano mkubwa na hifadhi ya mazingira.

(a) Kilimo na Mifugo:

Kilimo

Ardhi yenye rutuba na maji ya kutosha inahitajika ili kufanikisha kilimo.

Ardhi inayofaa kwa kilimo hupoteza rutuba yake kwa uchomaji moto holela, matumizi ya mbolea za chumvi chumvi kupita kiasi, uharibifu wa vyanzo vya maji na mmomonyoko wa ardhi.

Kwa kutumia mbinu za kisasa za Kilimo, ardhi huongeza tija kwa kila eneo linalolimwa. Mbinu hizi ni pamoja na:

- Kulima kwa kutumia matuta
- Matumizi ya mboji na samadi
- Kulima kwa kupumzisha ardhi kama eneo linaruhusu.

Ufugaji wa Wanyama

Moja ya shughuli za kujiletea maendeleo ni ufugaji wa wanyama kama vile ng'ome, mbuzi na kondoo. Hifadhi ya mazingira inaleta uhakika wa kuipatia mifugo malisho na maji ya kutosha.

Hifadhi ya mazingira inahitaji kuzingatia uwiano wa idadi ya mifugo na eneo la malisho lililopo. Idadi ya mifugo ikizidi uwezo wa eneo husababisha mmomonyoko wa udongo na upotevu wa rutuba. Kwa vile uoto wote wa asili (nyasi, majani) huliwa na mifugo hiyo na ardhi hubaki bila hifadhi yoyote, maji yenye mwendo wa kasi kutokana na mvua pamoja na upepo katika maeneo haya huondoa udongo wa juu kwenye ardhi hiyo ambao ndio yenye rutuba.

Ni muhimu kuzingatia ufugaji bora wenye lengo la kuhifadhi na kutumia ardhi vizuri ambayo huwezesha kutunza vyanzo vya maji na malisho kwa ajili ya mifugo.

(b) **Maliasili:**

Ufugaji Nyuki

Nyuki ni wadudu wenye manufaa mengi. Kwa mfano, hutupatia asali, nta, dawa, ajira na kuwezesha mimea kutoa mazao kwa kuifanya ibadilishane chavua. Kwa ajili ya kazi hii nyuki wanahitaji mazingira ambayo yatawafanya waendelee kuishi.

Kuvuna asali kwa kutumia moto husababisha uharibifu wa mazingira ya asili ya wadudu hawa.

Kukosa mazingira yanayostahili au sehemu ya kuishi husababisha nyuki kuhama.

Uvuvi

Uvuvi una manufaa mengi kwa binadamu kama vile kutupatia chakula bora, ajira kwa watu wanaoishi maeneo ya uvuvi, huleta fedha za kigeni na kutengeneza chakula cha mifugo.

Shughuli za uvuvi hufanyika katika maeneo yaliyo na mazingira ya maji kama vile mabwawa, malambo, mito, maziwa na bahari. Sehemu hizi zinahitaji kuhifadhiwa ili samaki waendelee kuwepo pia kwa vizazi vijavyo.

Uvuvi haramu wa sumu au baruti huharibu mazingira ya maji na kuua viumbe hai. Kujaa udongo na uchafu majini kunaweza kusababisha samaki wafe na kushindwa kuzaliana.

Misitu

Misitu ina faida nyingi, kwa mfano:

⇒ Misitu huyawezesha mazingira yafae kwa kuishi binadamu, wanyama, ndege, wadudu na viumbe hai wengine;

⇒ Husaidia kuhifadhi maji ardhini na hupunguza ukali wa mionzi ya jua kabla ya kufikia ardhi.

⇒ Hurutubisha udongo kwa ajili ya kilimo.

⇒ Hupunguza mmomonyoko wa udongo.

⇒ Huleta kivuli kwa wanadamu na wanyama.

⇒ Huvutia utalii.

⇒ Husaidia kuwepo kwa mvua ya kutosha.

Uchomaji misitu ovyo, uvunaji holela wa mazao ya misitu na kilimo cha kuhamahama husababisha kupungua kwa misitu na hatimaye kwisha kabisa. Kwa hali hiyo binadamu anahitaji kujenga mahusiano mazuri na misitu na pia kuihifadhi ili aendelee kunufaika nayo.

Wanyamapori

Wanyamapori huishi kwa kutegemea nyasi, majani, matunda ya miti na kujipatia maji katika maziwa, mabwawa, mito na madimbwi ambayo huwepo kwa kutegemea misitu.

Wanyama hao hurutubisha ardhi kutokana na vinyesi vyao.

Mazingira yanapoharibika wanyama hao hukosa usalama wa kuishi na hulazimika kuhama na kutafuta mahali pengine.

Uharibifu wa mazingira umesababisha wanyama wengi kudhoofika na kushindwa kuongezeka kwa kasi na baadhi yao kupoteza uhai na kutoweka.

Kuna umuhimu wa kuhifadhi mazingira ili wanyama pori waendelee kuwepo kwani hutumiwa na binadamu

kama rasilimali ya kumpatia chakula na fedha kwa njia zinazokubalika kisheria.

3. VYANZO VYA UHARIBIFU WA MAZINGIRA

Kimsingi harakati za binadamu katika kujiletea maendeleo bila kudhibiti athari zake ndiyo chanzo cha uharibifu wa mazingira. Kuna sababu kuu mbili za uharibifu wa mazingira:

Sababu za Kiasili za Uharibifu wa Mazingira

(a) Maumbile ya ardhi katika sehemu husika kama vile sehemu za milima na zenye mvua nyingi zinaweza kuwa na mmomonyoko mkubwa wa ardhi.

(b) Mvua nyingi katika sehemu za tambarare husababisha mafuriko.

(c) Ukame wa muda mrefu huathiri maisha ya watu, mimea na wanyama.

Sababu zitokanazo na Shughuli mbalimbali za Binadamu

(a) Wingi wa watu na mahitaji ya chakula:

⇒ Kilimo na ujenzi wa nyumba kutokana na ongezeko la watu husababisha kufyekwa kwa misitu ili kupata eneo la makazi na kilimo.

⇒ Ongezeko la watu linasababisha ardhi kutopumzika na hatimaye kuchakaa.

(b) Mila na desturi:

Matambiko na madawa mengi ya asili yanayosababisha uharibifu wa mazingira.

(c) Wingi wa mifugo:

Mifugo mingi kupita uwezo wa ardhi kuhimili ni chanzo cha uharibifu wa mazingira kama vile kuleta ukame, mmomonyoko wa ardhi na kuharibu uoto wa asili.

(d) Kufyeka au kukata miti:

Wakazi wengi wa vijijini na mijini hutegemea nishati itokanayo na miti. Hii inaashiria ukataji miti kwa kiwango kikubwa.

Aidha, yako mahitaji mengine ya mwanadamu ambayo husababisha ukataji miti ovyo kwa mfano mahitaji ya eneo zaidi la kulima, biashara ya mazao ya misitu, ujenzi wa nyumba na mbao.

(e) Biashara ya mazao ya misitu

Mazao hayo ni kama mbao na boriti kwa ajili ya ujenzi na nguzo za umeme, matunda, kamba, dawa, mafuta, gundi, kuni na mkaa.

Ongezeko la mahitaji ya mazao haya linatokana na ongezeko la watu, ambalo nalo hupandisha bei katika soko huria.

Hali hii husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na hatimaye mazingira kushindwa kutoa tena mazao hayo.

(f) Uvamizi wa ardhi mijini na vijijini:

⇒ Mijini

Kasi ya watu kuhama kutoka vijijini kwenda mijini inazidi kuongezeka siku hadi siku na hivyo, kuchangia katika uharibifu wa mazingira kwa kupitia uchafuzi wa hewa kutokana na nyumba kubanana kwa sababu ya upungufu wa viwanja.

Kwa sehemu kubwa ujenzi mijini unaendeshwa pasipo mpangilio na bila kuzingatia usafi wa mazingira; hivyo, husababisha uchafuzi kwa njia mbalimbali.

⇒ Vijijini

Uchimbaji wa madini ovyo husababisha uharibifu wa ardhi.

(g) Kilimo cha kutumia mbolea ya viwandani:

Matumizi ya mbolea ya viwandani hususan ya chumvi chumvi yakizidi kiasi hupunguza uwezo wa ardhi kutoa mazao mengi.

(h) Matumizi ya madawa ya mimea na mifugo:

Madawa yanayotumiwa kuua wadudu kwenye mimea na yale yanayotumika kuogeshea mifugo yanaweza kuathiri mazingira na afya za binadamu. Vyanzo vya maji vinaweza kuchafuliwa na kuleta athari.

Matumizi yake yasipodhibitiwa na masalia yake yasipotupwa katika sehemu zinazostahili yataleta madhara.

4. ATHARI KUTOKANA NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA

Kwa jumla uharibifu na uchafuzi wa mazingira huleta athari zifuatazo;

(a) Uzalishaji wa mazao hafifu kutokana na kudumaa kwa shughuli za maendeleo;

(b) Tija au kiwango cha uzalishaji kwa eneo na kwa kila mtu hupungua. Kupungua kwa chakula na mapato husababisha umaskini. Watu maskini waliodhoofika hawawezi kuzalisha mali na chakula cha kutosha;

(c) Hali ya jangwa huleta madhara mengine katika jamii kama vile njaa, mafuriko, ukame na hatimaye kuleta vifo na upotevu wa mali kwa kiwango kikubwa;

(d) Ukosefu wa maji safi na salama husababisha magonjwa mengi ya wanadamu kama vile minyoo, kuhara na matende; na

(e) Umaskini na uharibifu wa mazingira ni kama watoto mapacha, uharibifu wa mazingira huleta umaskini, vivyo hivyo umaskini huleta uharibu zaidi wa mazingira.

5. MBINU ENDELEVU ZA KUHIFADHI MAZINGIRA VIJIJINI/MIJINI

Ili kuwa na maendeleo endelevu hapana budi kuchukua hatua madhubuti za kuhifadhi mazingira ambamo shughuli za maendeleo hufanyika:

(a) Miradi na shughuli zote za maendeleo zinazotarajiwa kufanywa hazina budi kufanyiwa tathmini ili kubaini athari za shughuli hizo kwenye mazingira. Ushauri wa kitaalamu ni wa lazima.

(b) Programu za upandaji miti ni muhimu katika kuhifadhi mazingira. Shughuli hii ianzie ngazi ya kaya.

(c) Ni vizuri wananchi wote wazingatie na kuheshimu ushauri wa kitaalam katika kutekeleza shughuli za maendeleo, hususan:

⇒ Kilimo;

⇒ Ufugaji wa kisasa;

⇒ Uvunaji wa asali;

⇒ Kuongeza matumizi ya nishati mbadala; na

⇒ Kupunguza matumizi ya nishati zitokanazo na mazao ya misitu kama kuni na mkaa.

(d) Kusimamia matumizi bora ya ardhi na kuzuia uvamizi wa ardhi mijini:

Kila Kiongozi kwa kushirikiana na Idara husika hususan Ardhi ahakikishe kuwa maeneo yote kwenye sehemu yake yamepimwa na azuie wale wote wanaovamia viwanja na kujenga kiholela.

Kuwa na Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kwenye Ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa. Kama Kijiji hakina mpango wa matumizi bora ya ardhi, ni vyema Kiongozi kwa kushirikiana na wataalam walipo hususan Maafisa Kilimo, Mifugo na Maliasili na kwa msaada wa Ofisi ya Ardhi ya Wilaya, kuandaa mpango huo. Mpango wa matumizi bora ya ardhi ulioandaliwa kwa njia shirikishi na kutathmini namna ambavyo shughuli za maendeleo zinaathiri mazingira na hivyo, kuamua ni hatua gani zichukuliwe, utasaidia sana kuzuia uharibifu. Mpango huu katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji na Mtaa huonyesha aina ya matumizi ya ardhi na mpangilio wake. Matumizi haya ni kama:

⇒ Maeneo ya makazi, mashamba na huduma;

Haya ni maeneo ya makazi na mashamba yanayozunguka majengo, mandhari ya sehemu za burudani, mahali pa kutupa takataka na sehemu zilizo wazi;

⇒ Maeneo ya kilimo;

Haya ni maeneo ya kilimo cha aina mbali mbali na mwingiliano wake na shughuli nyingine kama ufugaji, na maeneo ya misitu.

⇒ Maeneo ya kuchungia;

Haya ni yale yaliyotengwa mahsusi kwa ajili ya uchungaji huria. Aidha njia za mifugo na sehemu za manywesheo huwekwa wazi kwa kila mhusika ili kuzuia mgongano.

⇒ Maeneo ya misitu;

Haya ni yale maeneo yaliyotengwa maalum kwa ajili ya kuhifadhi uoto wa asili na yana miti mingi.

Haya yanaweza kutengwa kulingana na hifadhi au matumizi yake kama vile upatikanaji wa mbao, kuni, mkaa, asali, miti shamba na wanyama.

⇒ Maeneo ya wanyamapori:

Maeneo haya hutengwa maalumu kwa ajili ya matumizi ya wanyamapori na mimea asilia. Viongozi katika ngazi ya Kijiji wakifuata utaratibu mzuri wa kugawa maeneo yao kwa kufuata mfano uliotolewa hapo juu, wataweza kuzuia kuwepo kwa uharibifu wa ardhi na migongano ya watumiaji mbalimbali.

(e) Matumizi sahihi ya madawa kwa mifugo na mimea:

Kiongozi anatakiwa kupata taarifa kamili kutoka kwa wataalam walioko Wilayani juu ya madawa yaliyoruhusiwa na kwa kushirikiana na wataalamu walioko katika eneo lake atoe taarifa kwa mamlaka husika tatizo linapojitokeza.

6. WAJIBU WA KIONGOZI WA KIJIJI, KITONGOJI NA MTAA KATIKA KUHIFADHI MAZINGIRA

(a) Kuandaa na kuhimiza wananchi katika shughuli za hifadhi ya mazingira;

Shughuli hizi ziwe za kudumu katika mipango yao ya maendeleo;

Kiongozi katika ngazi ya Kijiji, Kitongoji au Mtaa akishirikiana na viongozi wenzake na wataalam aandae taratibu na miongozo ya kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli za hifadhi bila bughudha;

(b) Kuwa mfano katika kutekeleza shughuli za hifadhi endelevu;

Kiongozi anatakiwa awe mfano katika utekelezaji wa mipango ya hifadhi ya mazingira. Mara nyingi Kiongozi huigwa kimaadili, kimawazo na kimatendo na wananchi anaowaongoza. Kama Kiongozi akijiingiza katika matendo ya uharibifu wa mazingira kama vile uwindaji haramu, uchomaji misitu, ukataji miti ovyo na kutozingatia masharti ya kilimo bora, wananchi anaowaongoza nao wataiga matendo hayo.

(c) Kuwa kiungo kati ya wananchi na Viongozi wa Kata na Halmashauri ya Wilaya ili waweze:

⇒ Kutafuta habari muhimu zinazoweza kutumiwa na wananchi wake katika eneo lake.

⇒ Kwa kushirikiana na wataalam na wananchi katika eneo lake, wote kwa pamoja wabaini matatizo ya mazingira yanayojitokeza na kupendekeza aina ya msaada wa kitaalam unaotakiwa ili kukidhi mahitaji ya shughuli za ufugaji, misitu na maliasili nyingine.

(d) Kuhakikisha kuwa sheria za hifadhi zinafuatwa:

⇒ Kiongozi ashirikiane na Viongozi na wataalam walioko kwenye ngazi za Wilaya, Kata na eneo lake katika kupata na kutafsiri sheria zinazohusu hifadhi. Idara husika ni maliasili, ardhi, kilimo, mifugo, maji, madini na mipango miji.

⇒ Kiongozi ashirikiane na wataalam wa sekta mbalimbali juu ya matumizi ya sheria hizi katika eneo lake.

(e) Kuziwezesha Kamati husika katika eneo lake la uongozi, kubuni mikakati ya kupambana na uharibifu wa mazingira. Hii ni pamoja na:

⇒ Kubaini namna ambavyo wananchi wanaweza wakanufaika na mazingira na hivyo kuachana na vitendo vya uharibifu wa mazingira.

⇒ Kubuni njia za kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira katika sehemu yake ya uongozi kwa sababu wananchi wanaweza kuvunja sheria za kuhifadhi mazingira kwa makusudi au kwa sababu za kijamii au kiuchumi,

⇒ Kubaini maeneo yanayostahili kutungiwa sheria ndogo.

(f) Katika kusimamia sheria na kanuni za hifadhi, Kiongozi ajiepushe na upendeleo au kujiingiza yeye binafsi katika vitendo hivyo.

7. HITIMISHO

Kipeperushi hiki, pamoja na mambo mengine, kinaonyesha dhahiri kwamba mazingira na maendeleo haviwezi kutenganishwa. Maendeleo endelevu hayawezi kupatikana bila matunzo na matumizi mazuri ya mazingira. Usafi wa mazingira ni usafi wa vitu vyote vinavyozunguka mwanadamu kama vile hewa, nyumba, maji na mifugo. Hivyo, Kiongozi ahimize wananchi katika eneo lake **WAYATUNZE MAZINGIRA ILI MAZINGIRA YAWATUNZE.**